

OFISI YA KUTATUA MIZOZO

Mwongozo Wako wa Upatanishi wa Elimu Maalum



Kuwa sehemu ya mchakato chanya

Mwongozo wa Upatanishi wa Elimu Maalum

Hati hii ina maelezo ya kukusaidia kufahamu mchakato wa upatanishi na kujiandaa kwa kikao cha upatanishi. Wataalamu wa Elimu Maalum wa ConsultLine wa ODR na wa Kushirikisha Familia wanapatikana kujibu maswali kwa kutuma barua pepe kwa consultline@odr-pa.org au kupiga simu (800) 879-2301.

Ufafanuzi Uliotumiwa katika Mwongozo Huu

Mwongozo huu unatumia neno “mtoto” kurejelea watoto wote kuanzia kuzaliwa hadi umri wa miaka 21 wanaopokea huduma za elimu maalum.

Mwongozo huu unatumia neno “shule” au “wafanyakazi wa elimu” kurejelea mashirika yote ya elimu na wafanyakazi wao wanaowahudumia watoto kuanzia kuzaliwa hadi umri wa miaka 21 wanaopokea huduma za elimu maalum

Matumizi ya neno “mzazi” katika Mwongozo huu hurejelea wazazi au walezi wa watoto wote kuanzia kuzaliwa hadi umri wa miaka 21 wanaopokea huduma za elimu maalum.

Katika Mwongozo huu, neno “wahusika” linarejelea familia na shule au wafanyakazi wa elimu.

Yaliyomo

Ukurasa

Utangulizi	1
Kwa nini nizingitie upatanishi?.....	2
Siku yako ya upatanishi.....	3
Kushiriki katika mchakato wa upatanishi.....	5
Kujiandaa kwa upatanishi	7
Maswali yanayoulizwa Mara kwa Mara.....	8
Hitimisho	10

UTANGULIZI

Uhusiano kati ya wazazi na shule unaweza kutatizwa wakati kuna sintofahamu na mgongano kuhusu mpango wa mtoto. Utafiti uko wazi kwamba wakati wazazi na shule wanapofanya kazi kwa pamoja, watoto wana matokeo bora zaidi ya elimu. Upatanishi wa elimu maalum ni hudumu inayotolewa na ODR kusaidia familia ya watoto wenye ulemavu na shule kutatua maoni yao tofauti kuhusu mpango wa elimu maalum wa mtoto. Ikiwa familia na shule watakubaliana kushiriki katika upatanishi, wasimamizi wa kesi wa ODR watapanga tarehe, saa, na mahali pa kikao cha upatanishi. Faida za upatanishi zimewekwa katika Mwongozo huu.

Mambo Matano ya Kukumbuka Kuhusu Upatanishi

- Upatanishi ni mchakato wa pamoja wa kutatua matatizo ambao unaweza kusaidia kuanzisha mchakato wa kuponya mahusiano mabaya na kurejesha malengo, kwa pamoja, kwa mafunzo ya mtoto.
- Upatanishi ni mchakato ambao unategemea utayari wa mzazi na shule kujadili hoja zao waziwazi na kwa uaminifu kwa matumaini ya kupata maafikiano kuhusu sehemu inayohangaisha.
- Uamuzi wa kutumia upatanishi ni wa kujitolea kabisa. Wazazi au wafanyakazi wa shule hawawezi kulazimishwa kushiriki katika upatanishi.
- Upatanishi unaweza kuombwa wakati wowote, hata wakati usikilizaji wa kisheria umeombwa au unaendelea. Wazazi hawaondoi haki zao kwa sababu ya usikilizaji wa kisheria kwa kushiriki katika upatanishi.
- Katika upatanishi, wahusika hufikia makubaliano kuhusu mpango wa mtoto kwa pamoja. Katika usikilizaji wa kisheria, afisa wa usikilizaji ataamua mpango wa mtoto utakuwa upi.

Vidokezo Muhimu Kuhusu Wapatanishi wa ODR

- Wapatanishi huwezesha majadiliano kati ya mzazi na shule kuhusu maoni tofauti waliyo nayo.
- Wapatanishi husaidia mzazi na shule kupata mambo yanayokubaliwa kuhusu mpango wa mtoto.
- Wapatanishi wamefunzwa katika mbinu za upatanishi na sheria ya elimu maalum.
- Wapatanishi hawana mapendeleo, ambayo ina maana kuwa hawana maoni kuhusu maoni tofauti ya mzazi na shule.
- Wapatanishi hawatendi kama watetezi au wawakilishi wa mzazi au shule.
- Wapatanishi hawatendi kwa njia yoyote ambayo inafaidi familia au shule.
- Wapatanishi huandika makubaliano kati ya mzazi na shule katika “makubaliano ya upatanishi”, ambayo ni hati iliyoandikwa inayofunga kisheria inayoelezea wazi yale mzazi na shule wamekubaliana.
- ODR hulipa mpatanishi moja kwa moja kwa kazi yake.

KWA NINI NIZINGATIE UPATANISHI?

Zingatia baadhi ya tofauti kati ya upatanishi na usikilizaji wa kisheria.

Muda

Unapomba upatanishi kupitia ODR, msimamizi wa kesi huwasiliana na mhusika yule mwingine kuhusu ombi lako. Kwa kawaida ndani ya siku 10 ya ombi, msimamizi wa kesi ataweka tarehe, saa, na mahali pa kikao cha upatanishi.

Ijapokuwa vikao vya upatanishi vimeratibiwa siku nzima, kwa kawaida hudumu saa tatu hadi tano. Upande ule mwingine, usikilizaji wa kisheria kwa kawaida uhitaji vikao kadhaa na vinaweza kuchukua miezi kutatua. Maandalizi ya mashahidi na ukusanyaji wa ushahidi wa kusikilizwa unaweza kuchukua muda mwingine kwa mawakili, familia na wafanyakazi wa wilaya ya shule.

Gharama

ODR hulipa gharama zote za mpatanishi na afisa wa usikilizaji na usikilizaji wa kisheria kuhusu wanafunzi wenye ulemavu. ODR hailipii ada za wahusika wa ziada ambao mhusika yeyote anaweza kuwaalika kwa kikao cha upatanishi au usikilizaji wa kisheria, kama vile watetezi wa wazazi, wataalamu wa elimu, au mawakili. Kwa sababu usikilizaji wa kisheria huchukua vikao kadhaa na kwa kawaida hujumuisha gharama za ziada, gharama kwa wahusika wote kuhusiana na muda na fedha zinaweza kuwa nyingi.

Kutoa Uamuzi

Upatanishi huwezesha utoaji wa uamuzi kusalia na watu wale ambao wanamjua mtoto vizuri: wazazi na walimu. Katika upatanishi, maamuzi yote kuhusu mpango wa mtoto hufanywa kwa pamoja na wazazi na wafanyakazi wa elimu. Makubaliano ya upatanishi yanaangazia yale mzazi na shule wamekubaliana. Mpatanishi haamui matokeo ya upatanishi. Kinyume chake, katika mchakato wa kisheria, maamuzi na amri zote kuhusu mpango wa mtoto hufanywa na afisa wa usikilizaji. Huenda matokeo yasiridhishe kwa familia au shule.

SIKU YAKO YA UPATANISHI

Lengo la sehemu hii ni kufafanua upatanishi wa kawaida. Tafadhali kumbuka kwamba ijapokuwa hii ni hali ya “kawaida”, mchakato wowote wa upatanishi unaweza kubadilika kulingana na mtindo na mapendeleo ya kibinafsi ya kila mpatanishi, na hata pia mahitaji ya wahusika.

Kupanga Siku Yako

ODR hufanya kazi na wahusika ili kupata tarehe na saa zinazokubaliwa na watu wote kwa kikao hicho cha upatanishi, hata jioni ikiwa wahusika wote watakubali. Kwa sababu ya ugumu wa kubainisha muda ambao kila kikao cha upatanishi kitachukua, inapendekezwa kwamba uweke siku nzima au jioni mapema kwa ajili ya mkutano huo. Washiriki wote wanaombwa kusalia hadi kikao kikamilike. Vikao vya kawaida vya upatanishi vinadumu kati ya saa tatu hadi tano.

ODR huwasiliana na wahusika ili kuwafahamisha kuhusu tarehe, saa na mahali pa upatanishi. Punde tu wahusika wanapopatia ODR orodha yao ya washiriki, ODR itatoa orodha hii kwa kila mhusika. Lazima shule ijumuishe mtu aliye na mamlaka ya kutoa rasilimali za kutatua sintofahamu hiyo. Familia zinaweza kuwaalika wahusika wengine katika upatanishi ili kuwasaidia, lakini watawajibikia ada zozote.

Kuanzisha Upatanishi/Utangulizi

Kikao cha upatanishi kitaanza moja kwa moja wakati uliowekwa. Mpatanishi atasalimiana, na ikihitajika, awatambulisha wahusika wote na wageni walioalikwa. Mchakato wa upatanishi na kanuni zitafafanuliwa. Umuhimu wa majadiliano wazi na ya uaminifu, kudumisha faragha, na umuhimu wa kila mhusika kujitolea kwa makubaliano yanayofunga husisitizwa na mpatanishi.

Taarifa za Ufunguzi

Mwakilishi kutoka kwa kila mhusika atapewa nafsi ya kuwakilisha maoni yake kuhusu matatizo. Kwa kawaida, taarifa za ufunguzi hutolewa na mzazi na Mkurugenzi wa Elimu Maalum au Mwakilishi wa LEA, lakini wahusika hubainisha hii hao wenyewe. Mpatanishi na wahusika wote watasikiliza bila kutatiza. Lengo la taarifa ya ufunguzi ni kumfanya kila mtu afahamu mitazamo yote ya maoni. Huenda mpatanishi akauliza maswali au kutoa muhtasari wa kilichosemwa.

Kikao cha Pamoja

Vikao vya pamoja, ikiwemo wahusika na wageni waalikwa, husaidia kutambua maeneo ya makubaliano na matatizo ambayo yanahitaji kujadiliwa na suluhisho zaidi. Kutokubaliana kwa uwazi na kwa adabu na mazungumzo yanahimizwa ili kupendekeza na kutathmini suluhisho zinazowezekana.

Kikao cha Faragha (Mkutano)

Huenda wahusika wakawa na nafasi ya kukutana kwa faragha na mpatanishi; mkutano huu wa faragha unaitwa mkutano. Lengo la mkutano huu ni kuwapa wahusika nafasi ya kuongea faraghani na mpatanishi bila mhusika yule mwingine kuwepo, ili kuelezea wasiwasi au matatizo. Mpatanishi hatashiriki maelezo kutoka kwenye mkutano huo na mhusika yule mwingine bila ridhaa.

Mapumziko ya Mpatanishi

Wakati ataona inafaa, huenda mpatanishi akapumzika ili kuangazia kivyake kilichofanyika katika kikao cha pamoja au mkutano ili kubainisha njia bora ya kuendelea na upatanishi. Huenda wahusika wakaomba pia mapumziko kwa sababu yoyote ile.

Uandishi wa Makubaliano

Ikiwa wahusika watapata suluhisho la matatizo, mpatanishi atawasaidia kuunda makubaliano yaliyoandikwa. Wahusika watabainisha sheria za makubaliano na kutunga maneno. Mpatanishi ataandika makubaliano hayo kwa ajili ya wahusika wote. Wahusika wote katika kikao cha upatanishi watatia saini makubaliano hayo. Nakala za makubaliano zitasambazwa kwa wahusika wote kama hati za mkutano huo.

KUSHIRIKI KATIKA MCHAKATO WA UPATANISHI

Mpatanishi:

- Atafafanua jukumu lake kama mwezeshaji ili kuwasaidia wazazi na walimu katika kupata makubaliano.
- Atasikiliza maoni ya kila mhusika kuhusu tatizo.
- Atasaidia kutambua matatizo ya kupatanishwa.
- Atatafuta taarifa kutoka kwa kila mhusika kuhusu msimamo wake wa elimu ya mtoto, atauliza maswali ya kufafanua, kama inavyofaa, ili kuhakikisha kila mtu anaelewa matatizo.
- Atasisitiza hali zilizopo za kutoelewana, kwa kutozungumzia mambo ya zamani na kuzingatia tu yale muhimu kwa ajili ya ufahamu na upangaji. Lengo la hii ni kulenga suluhisho bora, la moja kwa moja la kutoelewana huko.
- Inapofaa, atakutana faraghani na kila mhusika (unaoitwa mkutano) na kuheshimu uamuzi wa kila mhusika wa kama maelezo yaliyojadiliwa mkutanoni yanapaswa kushirikiwa katika kikao cha pamoja.
- Atawasaidia wahusika wote, atafanya maamuzi, ataandika mambo yanayokubaliwa, lakini hatatatua mzozo.
- Atakusanya, kukamilisha na kusambaza fomu zote zinazofaa kwa usimamizi wa ODR.
- Kwa kutumia lugha iliyotengenezwa na wahusika, mpatanishi ataandika makubaliano ya upatanishi, ambayo yatatiwa saini na wahusika wote, yakisema hasa wahusika walikubaliana nini.
- Ana mamlaka ya kusitisha kikao cha upatanishi ikiwa katika uamuzi wake wa kitaalamu, majadiliano haya mazao yoyote.

Wazazi:

Wanaweza kuwaalika washiriki (kama vile mtetezi, wakili, mshauri, daktari wa mwanasaikolojia) kwenye kikao ili kusaidia na mchakato wa upatanishi. Wazazi wanawajibika kwa ada zozote zilizotathminiwa na wageni wataalamu. Ikiwa mzazi atachagua kumleta wakili kwa upatanishi, huenda shule ikamleta wakili pia. Ikiwa mzazi ataamua kushiriki katika upatanishi bila wakili, shule hairuhusiwi kumleta wakili.

Wawakilishi wa Wilaya ya Shule au Wakala:

- Ni timu ya wataalamu watatu ambao wanafahamu vizuri mahitaji ya mwanafunzi. Lazima mwanachama mmoja awe na mamlaka ya kutoa rasilimali.
- Wasimlete wakili kwa kikao cha upatanishi ikiwa mzazi hamleti wakili.

Wazazi na Wawakilishi wa Wilaya ya Shule au Wakala:

- Hutenga siku nzima kwa ajili ya upatanishi, ijapokuwa kikao kinaweza kuwa kifupi.
- Hushiriki katika upatanishi kwa nia njema, kwa lengo la kupata maafikiano.
- Huwakilisha maoni yao, ikiwemo maelezo yote muhimu, kwa njia ya heshima.
- Huomba ufafanuzi wakati kitu hakijaeleweka.
- Hufanya mkutano na mpatanishi akiombwa/ikihitajika.
- Hutafuta nafasi za kutatua tatizo kwa pamoja.
- Huzingatia maoni ya wengine wakati wa kukagua hali zote za mpango wa mwanafunzi.
- Hushiriki kabisa katika kikao kwa uwazi wa fikra, hushirikiana ili kutoa mapendekezo, kukuza chaguo na kuunda makubaliano ya upatanishi.
- Hukamilisha tathmini ya kikao cha upatanishi.

Ofisi ya Kutatua Mizozo:

- Huwachagua na kuwafunza wapatanishi.
- Hutoa nyenzo za maelezo kwa wazazi, walimu, na watetezi wanaotaka upatanishi.
- Humteua mpatanishi baada ya wahusika kukubali kutumia upatanishi.
- Hutathmini na kufuatilia ufaafu wa huduma za upatanishi za wazazi na walimu katika Pennsylvania.
- Hulipia ada ya mpatanishi kwa ajili ya upatanishi kuhusu wanafunzi wenye ulemavu.
- Hukagua tathmini ya vikao vya upatanishi na hutoa maoni kwa wapatanishi kuhusu kila kikao cha upatanishi.
- Hutoa ripoti ya maelezo ya upatanishi katika Ripoti yake ya Kila Mwaka.

KUJIANDAA KWA UPATANISHI

Kupanga kikao

Weka wazi ratiba yako ya siku nzima. Hakikisha umeleta hati zote zinazohitajika. Panga maelezo yako na ushiriki nyenzo. Kutana na wageni uliowaalika kuhudhuria na ufikirie kuhusu mada zifuatazo:

- Mtoto
- Chaguo ambazo zinaweza kutatua tatizo
- Ulichu tayari kufanya
- Yale unataka mhusika mwingine kuzingatia

Wahusika wote wanaombwa kuhudhuria na kushiriki kwa fikra nzuri kuwadia kutatua tatizo.

Iwapo kuna hali ya dharura...

Iwapo hali ya dharura itafanyika siku ya upatanishi, wasiliana na ODR kwa 717-901-2145 au (800) 222-3353 haraka iwezekanavyo ili wengine waweze kuarifiwa. Ikiwa unapiga simu baada ya saa za kawaida za ofisi, acha ujumbe kwenye mashine ya kujibu.

MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA

Ni nani anaweza kuomba upatanishi?

Mtu yeyote anayehusika katika mpango wa elimu wa mtoto anaweza kuomba upatanishi. Kwa kawaida upatanishi huombwa na mzazi au Mkurugenzi/Msimamizi wa Elimu Maalum. Ikiwa mzazi ana wakili, wakili wake wanaweza kuomba. Vivyo hivyo, wakili wa shule anaweza kuomba upatanishi, lakini mzazi ataamua kama kwa kweli wakili atashiriki katika kikao cha upatanishi.

Lazima mzazi awe na wakili ili kushiriki katika upatanishi?

Hapana. Hadi 2021, mawakili hawakuwa wakiruhusiwa kuhudhuria upatanishi. Wakati mpango wa upatanishi wa Pennsylvania ulipotengenezwa mwaka wa 1986, lengo lake lilikuwa kuunda mdahalo ambapo wazazi na wafanyakazi wa shule wanaweza kutatua kutoelewana kivyao. Wazazi, wawakilishi wa shule, na mpatanishi pekee ndio wangehudhuria vikao vya upatanishi. Hata hivyo, sasa, ikiwa wazazi watachagua kwa gharama yao wenyewe kumleta wakili kwa kikao cha upatanishi, wanaweza kufanya hivyo. Shule au wakala wa elimu anaweza pia kumleta wakili iwapo atachagua kufanya hivyo. Ikiwa mzazi hataki kumleta wakili kwa kikao cha upatanishi, basi shule au wakala wa elimu hatamleta wakili pia.

Wakili wote wa wazazi watawapatia wateja wao hati ya “makubaliano ya ada”, inayoangazia jinsi wakili atafidiwa kwa kazi yake kwa wazazi. Kila wakili ana hati yake mwenyewe ya makubaliano ya ada.

Ni nani huamua ni masuala gani yatakayojadiliwa katika upatanishi?

Wahusika huamua ni masuala gani yatakayojadiliwa katika kikao cha upatanishi. Mpatanishi atawasiliana na wahusika kabla ya kikao halisi cha upatanishi ili kutengeneza orodha ya masuala ya kujadiliwa katika kikao cha upatanishi.

Ikiwa mzazi ana wakili, kwa nini asitatue tu kutoelewana huko katika usikilizaji wa kisheria badala ya upatanishi?

Ijapokuwa usikilizaji wa kisheria ni ulinzi muhimu wa utaratibu kwa wazazi, usikilizaji wa kisheria unachukua muda mwingi, mara nyingi huwa na ubishi, na maamuzi kuhusu mpango wa mtoto hufanywa na afisa wa usikilizaji, badala ya wale ambao wanamjua mtoto vizuri: wazazi na wataalamu wa elimu.

Je, ninaweza kuomba upatanishi ikiwa tayari nimeomba mchakato wa kisheria? Itakuwa aje ikiwa mchakato wa kisheria umeanza tayari?

Unaweza kuomba upatanishi wakati wowote ule, hata kama umeomba usikilizaji wa kisheria au hata kama upo katikati ya usikilizaji wa kisheria. Kukubali na kushiriki katika upatanishi hakutabadilisha muda katika usikilizaji wa kisheria, wala hautatatiza usikilizaji wa kisheria kwa njia yoyote ile. Kwa sababu upatanishi hufanikiwa sana, hata hivyo, huenda matokeo yakawa kwamba usikilizaji wa kesi hauhitajiki tena. Ikiwa hiyo itafanyika, mzazi au shule watumwarifu afisa wa usikilizaji. Huenda makubaliano ya upatanishi yakasema ni nani anaweza kumwarifu afisa wa usikilizaji.

HITIMISHO

Upatanishi ni chaguo linalolenga kutatua mizozo na kukuza mawasiliano bora kati ya wazazi na wafanyakazi wa wilaya ya shule kuhusu watoto walio na mahitaji maalum, wanaostahiki au wanaofikiwa kustahiki IEP, mpango wa 504, na/au GIEP. Kikao cha upatanishi kinawapa washiriki nafasi ya kuelezea maoni yao na kusikiliza maoni ya wengine katika mazingira yasiotishia, na yasio na uadui. Kupitia uwezeshaji wa upatanishi, wahusika wanaweza kuafikiana kuhusu masuala mahsusi na kupata njia ya kutatua matatizo ya baadaye, ambayo itasababisha mgongano kidogo na mahusiano bora ya kufanya kazi kwa watoto wanaowajali.

Ofisi ya Kutatua Mizozo inafuraha kwamba unashiriki katika mchakato wa upatanishi. Tunatumaini huu utakuwa uzoefu wenye ufanisi na mwema kwa watu wote. Ikiwa, kabla au baada ya kikao cha upatanishi, wazazi wana maswali kuhusu haki za elimu maalum za mtoto wao, wanahimizwa kupiga simu kwa ConsultLine ya Elimu Maalum, nambari ya simu isiyolipishwa (800) 879-2301. Mtaalamu atasaidia katika kufafanua haki na chaguo zinazopatikana.



OFFICE FOR DISPUTE RESOLUTION

6340 Flank Drive

Harrisburg, PA 17112-2764

(800) 222-3353 (717) 901-2145

WATUMIAJI WA TTY: PA Relay 711

www.odr-pa.org



pennsylvania
DEPARTMENT OF EDUCATION

Kupitia Ofisi ya Kutatua Mizozo, Idara ya Elimu ya Pennsylvania (PDD) inatimiza wajibu wake wa kisheria wa kudumisha mfumo wa mchakato wa kisheria wa elimu maalum. PDE hushirikiana na Central Susquehanna Intermediate Unit kutoa msaada wa hazina ya serikali na wa usimamizi wa ofisi hiyo, bila kuhusika katika shughuli muhimu.

The Central Susquehanna Intermediate Unit (CSIU) haitabagua katika mipango ya elimu, shughuli au ajira kwa msingi wa mbari, rangi, asili ya taifa, jinsia, ulemavu, hali ya ndoa, dini, mapendeleo ya kimapenzi, ukoo, uanachama wa chama cha wafanyakazi, au ainisho nyingine za kisheria zinazolindwa. Tangazo la sera hii linalingana na Title VI ya Sheria ya Haki za Wananchi ya 1964, Title IX ya Marekebisho ya Elimu ya 1972, Sehemu ya 504 ya Sheria ya Urekebishaji Tabia ya 1973, na Sheria ya Wamerikani wenye Ulemavu ya 1990. Wafanyakazi na washiriki wa mpango ambao wana swali au malalamiko ya unyanyasaji au ulemavu, au ambao wanahitaji maelezo kuhusu kuwakimu watu wenye ulemavu, wanapaswa kuwasiliana na Director of Human Resources, CSIU, 90 Lawton Lane, Milton, PA 17847, (570) 523-1155.